

Ilipofika jioni ng'ombe, mbuzi na kondoo walirudi kutoka malishoni.

Mfugaji aliwaongoza wote kuingia kwenye banda lao.



Sungura mjanja alikuwa macho kwenye banda akiwaza, "Ninataka kwenda nje." Sungura wengine walikuwa wamesinzia.




Ghafla mlango wa banda ulifunguliwa. Mfugaji alileta chakula.



Chakula kile kilinukia vizuri.
Sungura wote waliamka.
Wote walimsogelea Mfugaji.



Sungura Mjanja alimtazama Mfugaji. "Ahaa!
Najua nitatoka vipi. Lazima kesho nitoke.
"Aliwaza moyoni.



Sungura walikula na kushiba. Baada ya muda usingizi uliwapitia.



Ilipofika asubuhi, Mfugaji aliwaletea sungura chakula chao.

Sungura ,mjanja alisema moyoni, "Leo ni lazima nitoke bandani."

Sungura mjanja aliingia kwenye kapu la Mfugaji bila kuonekana.





Sungura mjanja alitoka ndani ya kapu akiwa na furaha. Aliimba huku akitembea kwa madoido. Ghafla mbele yake akatokea mbwa. Mbwa alibweka alipomwona Sungura mjanja.

Mbwa alianza kumfukuza Sungura mjanja.






**Mbwa alimfukuza lakini
Sungura mjanja alikimbia zaidi.**





Sungura mjanja alimwacha
mbwa, akaingia msituni.
Aliona majani mazuri. Alikula
majani mpaka akashiba.
Usingizi ukampitia.






Mara, Sungura mjanja aliamshwa na mngurumo wa simba. Simba alinguruma kwa sauti ya kutisha.




Simba yule alikuwa akitafuta chakula msituni. Simba alianza kumfukuza Sungura mjanja. Sungura mjanja alianza kukimbia.

Sungura mjanja alikimbia kwa nguvu zake zote, huku akiwaza, "Lo! Nitapona kweli leo?" Alikimbia usiku kucha. Hakujuua anakoelekea.



Kulipokucha, hakuamini. Alijikuta yuko karibu na nyumba ya Mfugaji. Jasho lilimtoka huku akihema sana.



Sungura mjanja alichoka na alikuwa na njaa kali. Mlango wa banda ulikuwa wazi. Mfugaji alikuwa akiwapa sungura wengine chakula.



Sungura mjanja alinyata na kuingia ndani.



Kwa sababu ya njaa
aliyokuwa nayo, alikula sana.
Sungura mjanja aligundua,
dunia ya nje ina raha na
taabu zake.



Tangu siku ile Sungura mjanja alikuwa mpole
na mshauri mzuri kwa wenzake.

